



Transcript: Haraka haraka.

- Kuluthumu: Amina huyo fundi wako anajua kushona nguo kweli?
- Amina: Ndiyo anajua.
- Kuluthumu: Maana hata hii nguo niliyoivaa kanishonea yeye anajua kweli.
- Kuluthumu: Je tukienda tutamkuta?
- Amina: Ndiyo tutamkuta, usikute ana kazi nyingi.
Shikamoo fundi.
- Fundi: Marahaba, hamjambo?
- Amina: Nimekuletea mteja mwingine mshonee nguo vizuri.
- Kuluthumu: Fundi hivi vitambaa ni vya harusi naomba nishonee vizuri.
- Fundi: Hamna shaka.
Ngoja nikupime, hapo unasemaje urefu ni sawa.
- Kuluthumu: Urefu, nataka iwe ndefu kabisa.
- Amina: Fundi fanya haraka basi nataka kwenda sokoni.
- Fundi: Usiwe na shida.
- Amina: Fundi mimi nina haraka, mbona unapima mara mbili mbili?
- Fundi: Mimi ni fundi.
- Amina: Mimi nachelewa fundi nataka kwenda sokoni.
- Fundi: Nataka nikushonee nguo upendeze.
- Amina: Mimi naenda fundi.

Fundi: Subiri sijamaliza kupima bado.

Amina: Mimi naenda fundi, sijaenda kununua mboga za jioni.

Fundi: Kwa hiyo mimi ninavyokupima siyo fundi tulia basi nimalize.

Amina: Nakuja kuchukua kesho asubuhi fundi.

Fundi: Watu wengine wanaharaka kweli!
Siku ya pili.

Amina: Shikamoo fundi nimekuja.

Fundi: Marahaba, hujambo?

Amina: Fundi umeshona vizuri kweli nitapendeza?

Fundi: Ndiyo utapendeza nimeshona vizuri.

Amina: Mimi nakuamini fundi haya asante kwaheri.

Fundi: Haya kwaheri fundi.
Siku ya tatu;

Kuluthumu: Habari za leo fundi?
Nadhani unanikumbuka.

Fundi: Ndiyo nakukumbuka.

Kuluthumu: Nimekuja kuchukua nguo yangu na kama umenishonea vizuri, nitakuwa nakuja hapa kila siku.

Fundi: Usiwe na shaka nimekushonea vizuri.

Kuluthumu: Haya fundi asante.

Fundi: Haya karibu tena.

Amina : Leo kwenye harusi nitacheza kweli.

Kuluthumu:

Utacheza wapi?

Kwanza nguo yako imebana, hata huwezi kucheza kwenye harusi.

Maana ulivyokuwa unamwuharakisha yule fundi afanye haraka haraka.

Amina:

Kweli kabisa subira ya vuta heri.

VOCABULARY

Msamiati.

Shaka = Wasiwasi = worry

Subira - Uvumilivu - patience